# TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

**HOTUBA YA KAIMU MKURUGENZI, DKT. K. A. NIHUKA KWA WAFANYAKAZI WA TEWW, UKUMBI WA KAWAWA, MAKAO MAKUU DSM, TAREHE 09/04/2018**

**APRIL, 2018**

**Ndugu Wafanyakazi wa TEWW**,

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwa hai siku ya leo. Huu ni mkutano wangu wa kwanza kama Kaimu Mkurugenzi wa TEWW, ambao tumeuitisha ili tufahamishane masuala muhimu yaliyotokea ndani ya Taasisi yetu na kwa pamoja tuweza kujipanga upya katika kutekeleza majukumu ya Taasisi.

Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuwajulisha rasmi kuwa aliyekuwa Mkurugenzi wetu wa TEWW, Dkt. Fidelice Mafumiko ameteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali, kuanzia tarehe 03.04.2018, tunashukuru Mungu kwa uteuzi wake, tunampongeza na tumuombee aifanye kazi yake mpya kwa ufanisi na mafanikio. Uteuzi wake ni fahari kubwa, kwa Taasisi, Wafanyakazi wote na Taifa kwa ujumla.

Kama mnavyofahamu, Dkt. Mafumiko amekuwa mfanyakazi wa TEWW kwa takribani miaka 10 sasa, akihudumu katika nafasi ya Naibu Mkurugenzi (Taaluma, Utafiti na Ushauri) na baadaye kama Mkurugenzi na Mtendaji Mkuu wa Taasisi. Amefanya mambo mengi katika kuchangia ustawi na maendeleo ya Taasisi. Tunampongeza sana kwa kuteuliwa kwake na kwa kweli tutamkumbuka daima. Dkt. Mafumiko alikwenda kuripoti katika majukumu yake mpya tarehe 06.04.2018 na atakapopata nafasi atakuja ili kuwaaga wafanyakazi wote wa TEWW. Vile vile, nipende kuchukua nafasi hii kuwajulisha kuwa kufuatia kuteuliwa kwake Dkt. Mafumiko amenikabidhi kukaimu ofisi ya Mkurugenzi wa TEWW rasmi kuanzia tarehe 04.04. 2018. Hivyo ni muhimu wajumbe wa Menejimenti ya

TEWW kutambua kuwa kwa sasa, mimi ndiyo Mtendaji Mkuu na ‘Chief Accounting Officer” wa Taasisi hadi hapo itakapotangazwa vinginevyo. Ingawa ninakaimu ninayo madaraka kamili ya Mkurugenzi na kwamba hakuna “vacuum” ya uongozi.

Naomba niwapongeze wafanyakazi wote pamoja na Menejimenti kwa kufanyakazi kwa kujituma katika Idara na Vitengo, vituo vya mikoa na Kampasi zote ambako kumewezesha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa TEWW hadi hapa tulipofikia chini ya uongozi wa Dkt. Mafumiko. Ninawaomba tuendelee kufanyakazi kwa pamoja na kwa kujituma na ushirikiano ili Taasisi yetu iendelee kung’ara. Pia ninawapongeza na kuwashukuru kwa dhati wakuu wa Idara na Vitengo, Wakufunzi Wakazi na wakuu wa Kampasi na Wafanyakazi wote niliokuwa nafanyanao kazi katika ofisi ya Naibu Mkurugenzi (Taaluma, Utafiti na Ushauri) kwa kujituma na kuwezesha kufikisha Taasisi yetu hapa tulipo. Ninafahamu, tumekuwa “tukikanyagana” hapa na pale, na hivyo nawasihi sana tuanze upya, tusameheane, na tuendelee kushirikiana zaidi kwa maslahi ya Taasisi yetu.

Napenda kuwafahamisha kuwa tumeachiwa Taasisi ikiwa haina Bodi ya Uendeshaji ya Taasisi kwani muda wake ulikwisha tarehe 03.04.2018. Hata hivyo mapendekezo ya Mwenyekiti wa Bodi na Wajumbe yamewasilishwa kwenye ngazi husika za uteuzi na tutaendelea kufuatilia ili tuwe na Bodi ya TEWW ndani ya muda mfupi.

Katika mazingira haya, maamuzi yote ambayo yangetakiwa yafanywe na Bodi itabidi tuwe tunawasiliana na ofisi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya

Elimu, Sayansi na Teknolojia na/au mamlaka nyingine kadiri tutakavyoona inafaa kwa ajili ya ushauri na maelekezo mbalimbali. Aidha, kwa maamuzi yanayofanywa katika ngazi ya Menejimenti, tutaendelea kushirikisha wajumbe wote wa Menejimenti kupitia vikao vyake katika kufanya maamuzi ya pamoja.
Ili kuongeza ufanisi wa ofisi ya Mkurugenzi na kuondoa mgongano wa kiutendaji, naomba menejimenti iridhie tuombe Katibu Mkuu Wizara ya Elilmu Sayansi na Teknolojia aridhie tukaimishe ofisi ya Naibu Mkurugenzi (Taaluma, Utafiti na Ushauri) kwa mfanyakazi atakayependekezwa. Hii itasaidia kuongeza ufanisi kwenye ofisi ya Mkurugenzi kwa kuwa kutakuwa na Manaibu wote wawili wakimshauri Mkurugenzi katika maamuzi mbalimbali ya siku kwa siku. Ni matarajio yangu kwa wajumbe wa Menejimenti mtaridhia pendekezo hili.

Katika kipindi nitakachokuwa nakaimu ofisi ya Mkurugenzi, napenda niwahakikishie wafanyakazi wote wa Taasisi kuwa tutasimamia kuhakikisha tunafanyakazi kwa kufuata maadili (values) ya Taasisi kama yalivyofafanuliwa kwenye Mpango Makakati wa TEWW, ukurasa wa 19 hadi wa 20. Maadili hayo ni pamoja na kufanyakazi kwa utaalam (Professionalism), uwasi (Transparency) uadilifu (integrity) na uwajibikaji (Accountability). Maadili mengine ni pamoja na kufanyakazi kwa ubunifu (innovativeness/creativity), kwa kujituma (hardworking), kwa kushirikiana (team working), kusaidia jamii (social responsibility), kujali jinsia zote (gender balance) na kupambana na utoaji au upokeajii rushwa ya aina yoyote (zero tolerance to corruption). Ni matarajio yangu kuwa tutaendelea kuzingatia maadili haya ili mara zote yabaki kuwa nuru

ya kuangazia utendaji kazi wetu wa kila siku katika Idara, Vitengo mbalimbali, Vituo vya mikoani na Kampasi zote.

Ndugu Wafanyakazi na wajumbe wa Menejimenti, katika kipindi nitakachokuwa nakaimu ofisi ya Mkurugenzi, napendekeza tuweke msisitizo katika kutekeleza maeneo yafuatayo ya Mapango Mkakati wa TEWW, (pamoja na mambo mengine);

**A. Mpango Mkakati wa TEWW**

1. Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati uliopo wa mwaka 2014/2015 – 2018/2019 pamoja na kuimarisha matumizi ya OPRAS katika utekelezaji wa majukumu ;
2. Kuhakikisha udurusu wa Mpango Mkakati unaendelea kwa ajili ya mwaka 2018/2019 - 2022/2023 unakamilika kwa wakati.

**B. Taaluma, Utafiti na Ushauri**

1. Kuendelea kufikisha fursa za elimu kwa wadau kupitia vituo vya ujifunzaji vya Wilaya (District Learning Centres) sambamba na kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji pamoja na kuongeza matumizi ya TEHAMA;
2. Kuendelea kuongeza udahili wa wanafunzi katika programu mbalimbali katika vituo vya Mikoa na Wilaya;
3. Kukamilisha Mkakati wa Kisomo na Elimu kwa umma pamoja na kuhimiza uanzishwaji wa vituo vya kisomo vya mfano kila mkoa;
4. Kuendelea kuhimiza shughuli za utafiti na uandishi wa makala za kitaaluma

5. Kuimarisha shughuli za ushauri wa kitaalamu pamoja na kuandaa mafunzo (semina) kwa wanataaluma ya namna ya kuandaa mapendekezo ya zabuni (consultancy service proposal writing).

**C. Maendeleo ya Wafanyakazi**

1. Kuendeleza mahusiano na mawasiliano mazuri baina ya wafanyakazi vyama vya wafanyakazi na Menejimenti ya TEWW kwa kuimarisha utamaduni wa kukutana na wafanyakazi kila baada ya miezi mitatu pamoja na kuhakikisha kuwa baraza la wafanyakazi linakutana kama ilivyopangwa;
2. Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi ya wafanyakazi wote pamoja na madarasa; na
3. Kuzingatia haki na stahiki za wafanyakazi kadiri ya miongozo mbalimbali.

***D. Huduma za Mikoani***

1. Kuendelea kuboresha ofisi na samani za vituo vya mikoa na Kampasi tukianza na vile vyenye majengo yanayomilikiwa na Taasisi.
2. Kushirikiana na viongozi wa mikoa kutafuta majengo kwa ajili ya ofisi za kudumu za Taasisi;
3. Kuanzisha ofisi na shughuli za Taasisi katika mikoa ambayo bado Taasisi haijafungua ofisi (mfano Njombe, Songwe, Katavi, Geita na Simiyu pamoja na Zanzibar);
4. Kuendelea kuimarisha Idara ya Utaratibu Vituo Mikoani kwa kuwapa vitendea kazi na ziara za mafunzo kwa kutembelea Idara kama hizo katika taasisi nyingine za elimu; na

5. Kuboresha utaratibu wa mgao wa pesa, kwa vituo vya mikoa kwa kutumia utaratibu wa bajeti badala ya maduhuli unaotumika hivi sasa.

**E. Mapato ya TEWW**

1. Kuongeza mapato ya ndani ya Taasisi kwa kuweka mikakati mizuri ya ukusanyaji ada ya mafunzo, ada ya uratibu na mapato mengine kwa kutumia TEHAMA; na
2. Kuimarisha udhibiti wa matumizi ya pesa za Taasisi na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuzingatia sheria za manunuzi na kanuni za fedha.

**F. Kujitangaza**

1. Kuhakikisha mkakati wa kujitangaza wa TEWW unakamilika na kuanza kuutekeleza mara moja;
2. Kutumia vyombo vya habari pamoja na tovuti ya TEWw kutangaza majukumu na shughuli za Taasisi
3. Kuandaa Taarifa ya Mwaka ya Taasisi (Annual Activity Report) na kuiwasilisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na kwa wadau wengine kila mwaka; na
4. Kuandaa "Facts and Figures" na kuwasilisha Wizarani na kwa wadau mbalimbali.

Ndugu Wafanyakazi na Wajumbe wa Menejimenti, bila shaka tumeshuhuudia matendo ya wizi na upotevu wa vifaa vya wafanyakazi na wanafunzi vinavyofanywa na watu ambao wakati mwingine wanatoka nje ya Taasisi. Tunahitaji kuwa na tahadhari katika maeneo

yote ya Taasisi kwa kuzuia watu wasioeleweka kuingia katika majengo yetu na magari tusioyajua kuegeshwa kwenye maeneo ya Taasisi. Ili kufanikishwa hili, walinzi wetu "NASA Security" wahakikishe wanadhibiti watu na magari kuingia katika maeneo ya Taasisi. Kwa upande wetu wafanyakazi na wanafunzi wote, ni muhimu tuvae vitambulisho muda wote wanapokuwa eneo la Taasisi.

Kwa kumalizia, naomba niseme kuwa hotuba hii pamoja na nyingine zitakazofuata zitakuwa zinapatikana kwenye tovuti ya Taasisi ndani ya masaa mawili baada ya kutolewa ili wafanyakazi wote, makao makuu na vituo vya mikoani na Kampasi waweze kuzisoma, kuzitafakari na kutekeleza maagizo na maelekezo mbalimbali. Rai yangu kwa wafanyakazi wote, ni kuwaomba tuendelee kushirikiana na kufanyakazi kwa bidii. Mungu Ibariki Tanzania Mungu Ibariki TEWW.

***ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA***